



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA
(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri)



Simu Na: 026 - 2702647
Fax Na: 026 - 2702203
Email: mkurugenzi.@iringamc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa,
S.L.P. 162,
IRINGA.

Kumb. Na. IMC/S.20/VOL.I/23

28.11.2022

TANGAZO LA AJIRA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa anapenda kuwatangazia nafasi za Ajira ya Mkataba wa miezi mitatu mitatu kwa watazania wenye sifa kama zifuatazo:-

MKUSANYA USHURU (MAKARANI) - NAFASI 50

SIFA:

- i. Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi katika mitaa,kata na vianzia mbali mbali vya mapato.
- ii. Awe na akili timamu na muadilifu.
- iii. Awe na kitambulisho cha utaifa NIDA.
- iv. Awe na Elimu ya Kidato cha NNE na kuendelea.
- v. Mwombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- vi. Awe na uwezo wa kutumia simu janja/POS.
- vii. Mwombaji aambatishe maelezo yake binafsi (CV).
- viii. Mwombaji aambatishe nakala ya vyeti vya (Taaluma). Cheti cha Kidato cha IV/VI, Cheti cha Kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni na ziandikwe majina kwa nyuma, nakala hizo zithibitishwe na Hakimu au Wakili.
- ix. Awe na wadhamini watatu wenye mali zisizohamishika
- x. Asiwe muajiriwa wa serikali

KAZI NA MAJUKUMU: -

- i. Kukusanya mapato katika kituo atakachopangiwa
- ii. Kutunza kumbukumbu za hesabu
- iii. Kutunza vizuri mashine za kukusanyia mapato (POS)


- iv. Kutoa na kuwasilisha makusanyo ya kila siku ya Halmashauri
- v. Kuwasilisha makusanyo katika Akaunti ya Halmashauri
- vi. Kufanya kazi zote atakazopangiwa na msimamizi wake

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **10 Disemba, 2022 Saa 9:30 Alasiri.**

MSHAHARA NI SHILINGI 150,000 KWA MWEZI

Maombi hayo yatumwe kwa anwani ifuatayo;-

MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA,
S.L.P. 162,
IRINGA.



.....
Dr. Stephen A. Ngwale

**KAIMU MKURUGENZI WA HALMASHAURI
MANISPAA YA IRINGA**

**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
IRINGA**